**Endeleza insha ifuatayo kwa maneno yako mwenyewe.**

*Mwandikie rafiki yako barua ukimwelezea njia kadhaa za kuupita mtihani wake wa mwisho wa muhula.*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kawaida ya binadamu __1__ yule, huomba Mungu ampe kile __2__ hana. Miongoni mwa yale binadamu huomba ni kujaliwa na mtoto. Mtoto ni muhimu katika maisha. Naye mtoto sharti __3__ wazazi na watu __4__ umri. Aidha aonyeshe heshima anapowaamkua asubuhi au jioni kwa kuwasalimia __5__. Mtoto wa aina hiyo __6__ hufaulu katika maisha __7__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** yoyote | **B.** yote | **C.** yeyote | **D.** wowote |
| **2.** | **A.** ambayo | **B.** ambacho | **C.** ambalo | **D.** ambazo |
| **3.** | **A.** aheshimiwe | **B.** amheshimu | **C.** awaheshimu | **D.** akuheshimu |
| **4.** | **A.** waliyomzidi | **B.** waliyemzidi | **C.** wanamzidi | **D.** waliomzidi |
| **5.** | **A.** shikamoo | **B.** sabalkheri | **C.** hamjambo | **D.** masalkheri |
| **6.** | **A.** hata hivyo | **B.** aghalabu | **C.** ingawa | **D.** sembuse |
| **7.** | **A.** yake | **B.** zake | **C.** lake | **D.** wake |

Mtoto mwenye tabia __8__ hufanya vyema katika mitihani yake huku walimu wake __9__ kwa kazi nzuri. Hata hivyo, iwapo mtoto mwenyewe atakuwa __10__, basi hataepuka kupewa __11__ mara kwa mara. Ikiwa hilo __12__ hakuna __13__ kwa ikabu kama hizi, maadamu __14__. Hatakuwa na wa kulaumu ila yeye __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | **A.** zuri | **B.** jema | **C.** mzuri | **D.** nzuri |
| **9.** | **A.** wakimpa mkono wa tahania | | **B.** wakimpa mkono wa tanzia | |
| | **C.** wakimpa mkono wa buriani | | **D.** wakimpa mkono wa urefu | |
| **10.** | **A.** jasiri | **B.** mjasiri | **C.** mjeuri | **D.** mwongofu |
| **11.** | **A.** adabu | **B.** viboko | **C.** adhabu | **D.** chungu |
| **12.** | **A.** itatokea | **B.** zitatokea | **C.** yatatokea | **D.** litatokea |
| **13.** | **A.** atakayemhurumia | **B.** atakayekuhurumia | **C.** atakayenihurumia | **D.** atakayewahurumia |
| **14.** | **A.** hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe | | **B.** kila chombo kwa wimbile | |
| | **C.** maji yakimwagika hayazoleki | | **D.** msiba wa kujitakia hauna kilio | |
| **15.** | **A.** yenyewe | **B.** mwenyewe | **C.** lenyewe | **D.** chenyewe |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** ***Tumia 'amba'***

Wadudu waliopigwa dawa jana wamekufa.

A. Wadudu ambao waliokufa waliopigwa dawa jana wamekufa.

B. Wadudu ambao wapigwao dawa jana walikufa.

C. Wadudu ambao watakaopigwa dawa jana watakufa.

D. Wadudu ambao walipigwa dawa jana walikufa.

**17.** Mtu anayehudumu ofisini kwa kutumwa kupeleka habari au ujumbe huitwaje?

A. Katikiro

B. Mnasibu

C. Mhazigi

D. Mhariri

**18.** Ainisha maneno yaliyopigiwa kistari:

Mtoto huyu ni wangu yule pale ni wako.

A. kivumishi, kielezi

B. kiashiria, kielezi

C. kivumishi, kiwakilishi

D. kielezi, kiwakilishi

**19.** ***Kanusha:***

Tungalifua nguo mapema zingalikauka.

A. Tusingalifua nguo mapema zisingalikauka.

B. Tusingalifua nguo mapema zisingekauka.

C. Tusingalifua nguo mapema hazingekauka.

D. Tusingefua nguo mapema zisingekauka.

**20.** Koma hutumika kwa njia hizi zote isipokuwa

A. tunapoandika anwani.

B. mwishoni mwa sentensi.

C. kutenganisha maneno katika orodha.

D. kutenganisha sentensi zenye masharti.

**21.** Kaka yake dada huitwaje?

A. Mwamu

B. Mkoi

C. Umbu

D. Mpwa

**22.** Jaji amemfunga babu kwa miaka ishirini.

***(Badilisha sentensi hii katika kauli ya kutendwa)***

A. Jaji amefungwa na babu kwa miaka ishirini.

B. Babu amefungiwa na jaji kwa miaka ishirini.

C. Jaji amefungia babu kwa miaka ishirini.

D. Babu amefungwa na jaji kwa miaka ishirini.

**23.** ***Andika kwa ukubwa:***

Mbwa huyu amemuuma mbuzi.

A. Jibwa huyu amemuuma mbuzi.

B. Kijibwa hiki kimekiuma kibuzi.

C. Jibwa hili limeliuma buzi.

D. Mbwa hawa wamewauma mbuzi.

**24.** ***Tegua kitendawili:***

Vuta huku nivute huku mwenzetu ateketee.

A. Msumeno

B. Ugwe

C. Moto

D. Njiti za kiberiti

**25.** Chagua orodha yenye viunganishi pekee.

A. Mbali, bali, hewala, kefule.

B. Chafu, maridhawa, hodari, bora.

C. Kata, nya, kanusha, jaza.

D. Seuze, aghalabu, maadamu, licha ya

**26.** Akisami $\frac{6}{8}$ huitwa

A. thumuni sita

B. thuluthi tano

C. sudusi tano

D. humusi sita

**27.** ***Majina yafuatayo yako katika ngeli gani?***

Mwiko, mwaka na muundi

A. U - I

B. I - I

C. I - ZI

D. LI - YA

**28.** Malipo ya kustaafu huitwaje?

A. Machorombozi

B. Kiinuamgongo

C. Zawadi

D. Fola

**29.** Chagua sentensi iliyoandikwa katika hali ya mazoea.

A. Wingu limetanda angani

B. Mgeni ajaye hukaribishwa vyema.

C. Tungalikataa kuwasaidia wangelihisi vibaya.

D. Ukipewa mwongozo utaiweza kazi yoyote.

**30.** ***Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa:***

"Kesho tutaenda kwetu tumwone mzazi wako," alimwambia.

A. Alimwambia kuwa kesho tutaenda kwao tumwone mzazi wake.

B. Alimwambia kuwa kesho wangeenda kwao kumwona mzazi wake.

C. Alimwambia ya kwamba siku iliyofuata wangeenda kwao wamwone mzazi wake.

D. Walimwambia kuwa siku itakayofuata wangeenda kwao kumwona mzazi wake.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Naam, husemekana asiyesikia la mkuu hupata makuu. Kwa ufupi yeyote asipojitenga au kujibari na maovu atahasirika. Hivyo basi <u>tunashauriwa kuambaa maovu kama kinyamkera</u>. Bozi alikuwa jamaa ambaye hakuijua methali hii na iwapo aliijua aliamua kuipuuza. Bozi alikuwa mkaidi kuliko hata mkia wa nguruwe. Kutokana na ukaidi huu, Bozi alikosa mengi sana maishani. Licha ya ukaidi wa Bozi, masomoni aliuma uzi kwelikweli. Alikuwa wembe unaokata kuwili. Baada ya Bozi kufanya vizuri katika shule ya msingi alipata mwaliko wa kujiunga na shule ya kitaifa ya Hekima. Kumbe hapo ndipo <u>maisha yake yalianza kuingia ufa</u>.

Hali hii ilitokana na ushawishi wa wanafunzi wenzake. Bozi akiwa katika kidato cha pili alianza kutumia unga ambao mwishowe ilimbainikia kuwa ulikuwa dawa za kulevya. Amliwaye nguo huchutana. Nao wazazi wake walijaribu kumwonya lakini alikaidi. Aliendelea na tabia hiyo hadi alipofumaniwa na mwalimu mkuu na kutimuliwa shuleni. Husemekana baada ya radi huja mvua. Baada ya masomo yake kufika hatima ya ghafla, alijiingiza katika wizi licha ya kuvuta hashishi.

Naam, yalikuwa majira ya jioni. Nilikutana naye na aliponiona alianza kuangua kicheko kirefu ungedhani mwendawazimu. Nilipoona hivyo woga ukanivaa kama lubega. Ilinibidi niharakishe nikijiendea zangu. Nilipofika nyumbani nilipokea habari kuwa Bozi alikuwa ametiwa mbaroni. Sikuwa na jingine ila kwenda kumtazama katika seli ya polisi alikokuwa amefungwa. Aliponiona machozi yalimtiririka njia mbilimbili kisha kwa huzuni nyingi akasema, "Laiti ningaliusikiliza wosia wa mama yangu leo hii singekuwa katika mahali hapa."

Hapo nilimsikitikia sana. Nilimpa pole na kumhakikishia kuwa siku moja angekuwa huru. Baada ya wiki moja nilifika kortini kusikiza kesi yake. Kwa wakati huu alikuwa ametulia tuli kuliko maji mtungini.

Baada ya dakika ishirini hakimu aliingia. Alichukua nafasi yake. Wote waliokuwa kortini wakanyamaza. Naam, kaa akiinua ganda mambo yamekatika. Ulifuata ukimia wa makaburini. Hakimu aliinua macho yake juu ya miwani na kumtupia Bozi.

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com

"Bozi kulingana na ushahidi uliotolewa, mahakama hii imekupata na hatia ya kulangua dawa za kulevya. Imekufunga kifungo cha mwongo mmoja na upewe kazi ya sulubu. Sote tuliokuwa ukumbuni tulinyamaza na kuelewa kuwa uhalifu haulipi chochote.

**31.** Hii ni tamathali gani ya lugha? Tunashauriwa kuambaa maovu kama kinyamkera.
A. Tashbihi
B. Istiara
C. Chuku
D. Kinaya

**32.** Kutokana na Bozi kuwa mkaidi,
A. alikoza maendeleo maishani mwake.
B. aliweza kuwa na maisha mazuri yaliyomwezesha kufurahia.
C. alikuwa kielelezo bora kwa vijana.
D. aliweza kuongoza katika mtihani wake wa kidato cha nne.

**33.** Maisha ya Bozi yaliingia ufa. Hii ina maana ya kuwa
A. maisha yake yalianza kupata matatizo.
B. maisha yake yalianza kubadilika.
C. maisha yake yalianza kuporomoka.
D. maisha yake yalianza kuharibika.

**34.** Ni wazi kuwa marafiki wa Bozi katika shule ya upili
A. walikuwa wasomi wa hali ya juu.
B. walikuwa hawazingatii masomo.
C. walijaribu kumwonya Bozi lakini akakaidi.
D. hawakutaka uhusiano wowote na Bozi.

**35.** Bozi,
A. alianza kutumia hashishi huku akijua.
B. hakuwa na habari kuwa alikuwa ameanza kutumia dawa za kulevya.
C. aliweza kusikiliza maonyo ya wazazi wake.
D. aliruhusiwa na wazazi wake kutumia dawa za kulevya.

**36.** Kisomo cha Bozi kilifika mwisho ghafla
A. baada ya kukosa walimu wa kumfundisha.
B. baada ya walimu kugoma kwa muda mrefu.
C. baada ya kukosa karo.
D. baada ya kufurushwa kwa kutumia dawa za kulevya.

**37.** Makala haya yameonyesha kuwa
A. Bozi alifurahia uamuzi wake wa kawaida wa wazazi wake.
B. Bozi alijutia uamuzi wake wa kutowaheshimu wazazi wake.
C. Bozi hakuwa na mwao kuwa dawa za kulevya ni mbaya.
D. Bozi alishikwa na polisi kimakosa.

**38.** Msimulizi alipokutana na Bozi akaanza kuangua kicheko angemsalimia vipi?
A. Sabalkheri
B. Masalkheri
C. Chewa
D. Makiwa

**39.** Kazi ya sulubu ni
A. kazi inayohitaji nguvu nyingi.
B. kazi ya kulazimishwa.
C. kazi ya kufanya kwa zamu.
D. kazi isiyo na malipo ya juu.

**40.** Kichwa mwafaka zaidi kwa makala haya ni
A. Bozi aachiliwa huru.
B. Asiyesikia la mkuu huvunjika mguu.
C. Bozi na ujinga wake.
D. Polepole ndio mwendo.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Wahenga walisema afya ni bora kuliko mali. Kile wahenga walichomaanisha ni kuwa unaweza kuwa na mali lakini iwapo afya imekupiga kumbo, basi mali yako si lolote si chochote. Mtu mwenye afya nzuri huwa na nguvu za kumwezesha kuendeleza maisha yake kikamilifu bila kizingiti. Katika hali hiyo, mtu huwa na uwezo wa kutenda kazi ili kujitafutia riziki, kupata mavazi, chakula na maskani bora. Haya yote huwezekana pale tu afya huweza kupewa kipaumbele.

Binadamu amekuwa na maadui wengi tangu kuumbwa kwake. Afya ya binadamu hasa imepokea maadui wengi. Miongoni mwa maadui wa afya ya binadamu ni ugonjwa wa ukimwi. Mashambulizi na upenyo wa ugonjwa wa ukimwi. Mashambulizi na upenyo wa ugonjwa huu mwilini hudhoofisha na hatimaye kusababisha kifo. Hakika ni kuwa gonjwa hili halina tiba. Japo kinga ipo, wengi wamejitia hamnazo tu. Kila siku tunaomboleza vifo vya marafiki na wanajamii. Njia ya pekee ya <u>kudhibiti</u> ugonjwa huu ni kunyosha tabia zetu.

La muhimu kujua hapa ni kuwa ugonjwa wa ukimwi hauna tiba. <u>Ugonjwa huu hauna huruma</u>. Ni zimwi lililojihami na kujizatiti kufutilia mbali sura za watu duniani. Hautambui wadogo wala wakubwa. Si walalaheri si walalahoi, si wanene tipwatipwa wala wakondefu kama mwiko wa pilau. Hautambui wafupi wala warefu kama unju. Uwe mwenye nguvu za kifaru ama mnyonge kama utumbo wa samaki. Dunia imeanza kuona idadi kubwa ya mayatima na wajane kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ukimwi. Makundi haya husalia bila furaha yoyote na maisha yao kusalia kuwa shehena kubura isiyoweza kubebeka kwao wenyewe.

Ukweli ni kuwa ugonjwa huu umegeuza furaha kuwa kilio, raha kuwa dhiki na wingu la simanzi kugubika umma. Wataalamu wanaendelea kuuma uzi katika harakati za kusaka na kusakanya tiba. Zaidi ya kufanya mapenzi kiholela, ugonjwa huu aidha huweza kusambazwa kwa mtu kuongezewa damu iliyo na virusi hivyo. Anapohitaji kufanyiwa matibabu ya kumwongezea damu, binadamu yu katika hatari ya kuambukizwa ukimwi endapo uangalifu hatuazingatiwa na wauguzi. Inatambuliwa kuwa mtoto tumboni mwa mamake anaweza kuambukizwa ukimwi na mama aliye na virusi hivyo. Mama kama huyo hafai kumnyonyesha mwanawe anapojifungua.

Vijana wanaotumia dawa za kulevya vilevile wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa virusi hivyo. Haya kutokana na matumizi ya sindano moja kujidungia dawa hizi. Iwapo mmoja wa wanaotumia sindano hiyo ana virusi, basi bila atiati wengine wote wataweza kuambukizwa maradhi hayo. Namna ya kuambukizwa maradhi hayo ni anuai na chungu. Ni vyema kila mmoja afahamu njia hizo ili aweze kujikinga na maradhi haya.

Ukweli ni kuwa, dalili za ugonjwa wa ukimwi zinaweza kujificha na kukolea mwilini kwa muda mrefu sana, hata zaidi ya miaka kumi. Athari zake zinapoanza kudhihirika waziwazi chombo huwa kilivuja zamani. Athari zinazoletwa na ukimwi ni anuwai na ni jukumu letu kujifunga kibwebwe kukabiliana na madhara yake.

41. Aya ya kwanza inaonyesha
A. ubaya wa kuwa na mali nyingi.
B. ubaya wa kuwa na uzima wa afya.
C. ni vizuri kuwa na mali hata kama afya si mzuri.
D. ya kuwa afya ndicho kitu cha thamani sana katika maisha ya binadamu.

42. Mtu akiwa katika hali nzuri ya afya, huweza kufanya yafuatayo ila
A. kujitafutia riziki.
B. kutafuta mavazi.
C. kushiriki katika mchezo wa kamari.
D. kutafuta makao mazuri.

43. Kulingana na kifungu ni njia ipi isiyoweza kueneza maradhi ya ukimwi?
A. Mtu kuwa na marafiki wengi.
B. Mgonjwa kuongezewa damu isiyochunguzwa kikamilifu.
C. Mama mwenye maradhi ya ukimwi akimnyonyesha mtoto wake mchanga.
D. Waathiriwa wa ugonjwa wa ukimwi kutumia sindano moja na wasio wagonjwa.

44. Madhara <u>makuu</u> zaidi yanayoletwa na ugonjwa wa ukimwi ni
A. watoto wengi kubaki kuwa mayatima.
B. vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wenyewe.
C. huzuni inayoletwa kwa wanaowahudumia waathiriwa wa ugonjwa huu.
D. hasara ya pesa nyingi kutumiwa katika kuhudumia wagonjwa.

45. Hii ni tamathali gani iliyotumiwa katika kauli hii: ***Ugonjwa huu hauna huruma***
A. Tashbihi
B. Tashhisi
C. Chuku
D. Ishara

46. Ili kuweza kupambana na ugonjwa wa ukimwi kila mmoja anahitajika kufanya nini kwa mujibu wa kifungu?
A. Kuzuia njia zozote zinazoweza kuhatarisha maisha.
B. Kuhakikisha mtu ameichunguza vizuri sindano anayoitumia kujidungia dawa za kulevya.
C. Kutofanyia uchunguzi damu zote tunazotiwa katika miili yetu.
D. Wanawake wote wajawazito kujifungulia nyumbani.

47. **<u>Kudhibiti</u>** ina maana ya
A. kuzuia
B. kuwezesha
C. kuchunguza
D. kuelewa

48. Aya ya <u>tatu</u> imedhihirisha kuwa
A. watu wanaelewa wazi athari za ugonjwa wa ukimwi.
B. hakuna mja aliye na ufahamu kuhusu ugonjwa wa ukimwi.
C. watu wanajua madhara ya ukimwi lakini wanajifanya hawaelewi chochote.
D. kila mmoja anaweza kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

49. Wingu la simanzi inamaanisha
A. matatizo mengi.
B. huzuni nyingi.
C. usingizi mwingi.
D. magonjwa mengi.

50. Kulingana na aya ya mwisho,
A. ili tuangamize ugonjwa wa ukimwi, kila mmoja sharti awajibike.
B. ugonjwa wa ukimwi hulemea zaidi wale walio na umri mdogo.
C. wengi wanaoathirika na ukimwi ni kwa kupenda kwao.
D. dalili za ugonjwa wa ukimwi hudhihirika punde mtu anapoambukizwa.

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com